# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

## FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MBONDOLE

S. L. P 15434,

DAR ES SALAAM.

MOB: 0784876958 **Mkuu wa shule**

0789609988 **Makamu mkuu wa shule**

0764433368 **Mtaaluma**

Tarehe …………………………

Kumb. Na. MBD/SEK/F1/2024/…………………………………..

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………..

S. L. P ……………………………………………….

……………………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBONDOLE ILIYOPO HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM MWAKA 2026.**

### 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA KWANZA**

(HOSTEL/KUTWA) katika shule hii mwaka 2026. Shule ya Sekondari Mbondole ipo umbali wa **KM 65** kusini mwa Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam. Ukiwa **Mbezi Terminal** utapanda magari ya **Gongo la Mboto**. Kisha **Gongo la Mboto – Viwege**, halafu **Viwege – Mbondole Sekondari** kwa bodaboda. Pia shule inafikika kupitia **Mbagala – Mbondole mwembeni**, halafu **Mbondole**

**Mbwembeni – Mbondole Sekondari** kwa bodaboda. Ukiwa **Chanika** unaweza kupitia **Chanika – Italian** kisha **Italian – Mbondole Sekondari** kwa bodaboda. Au **Chanika – Mbondole mbwembeni** kisha **Mbondole mbwembeni – Mbondole Sekondari** kwa bodaboda.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **05/01/2026.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 05/01/2026 na mwisho wa kuripoti ni tarehe **12/01/2026** ndani ya siku saba.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2. 1 Sare za shule

a) Sare za shule hii ni suruali 2 za kaki, mashati 2 meupe mikono mifupi kwa wavulana, sketi na blauzi/nusu kanzu 2 nyeupe. Maelezo ya mshono ni suruali ndefu chini 16 mzunguko, sketi inayogusa nyayo za miguu. Mshono wa sketi ni rinda box.

b) Mwanafunzi anaevaa juba atatakiwa kushona juba jeupe refu kufunika kifua hadi usawa wa mikono na atashona nusu kanzu isiyobana na inayofunika makalio (**kitambaa cha mfano kitatolewa shuleni**).

**NUKUU: KWA WANAFUNZI WANAOVAA JUBA HAWARUHUSIWI KUVAA SHATI LA MIKONO MIFUPI NA KUCHOMEKEA NUSU KANZU.**

c) Sweta dark green moja (1), soksi nyeusi pea mbili (2) na viatu vyeusi vya kamba na kisigino kwa wavulana, wasichana viatu flat shoes visiwe na kisigino kikubwa (juma na roza) na soksi nyeupe pea 2 (**viatu vyote kwa wasichana na wavulana viwe vya ngozi**)

d) Sare ya michezo kwa shule hii ni tracksuit za bluu kwa wavulana na wasichana na raba za michezo nyeupe kwa wote

2.2 Daftari counter book kumi (10) quire 4, kalamu na mkebe wa hesabu

2.3 Nauli ya kwenda shule na kurudi nyumbani pamoja matibabu kwa wanafunzi wa kutwa ni jukumu la mzazi.

2.4 Nauli ya wanafunzi wa hostel kwenda shule na kurudi nyumbani wakati wa likizo, matibabu, godoro, na vifaa vya malazi ni jukumu la mzazi/mlezi kwa wale wa hostel tu. *Pitia fomu ya hostel yenye mahitaji ya hostel*

2.5 Faili moja ya kutunzia nyaraka za mwanafunzi

2.6 Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kadi ya **bima ya afya** kwa ajili ya matibabu.

2.7 Vifaa vya usafi kwa wote

Ni wajibu wa mzazi kuhakikisha kwamba mwanafunzi anakuja na ufagio mrefu wa chelewa wenye mpini wa kufagilia uwanja na (kwanja/panga/jembe) kwa ajili ya kufanyia usafi na kazi za shule.

## 3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

**3. 1** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **Na.25** ya mwaka 1978 kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa sheria **Na.10** ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo yamsingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni jambo la lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

3.2 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi, uvutaji sigara na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
e) Kupiga au kupigana
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuwa mja mzito/kuharibu mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0 Mambo mengine yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

**4.1** Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali

**4.2** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

**4.3** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule

**4.4** Picha 2 passport size za wazazi/walezi

**4.5** Passport size 2 za mwanafunzi

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kwa kikamilifu**

**KARIBU MBONDOLE SEKONDARI**

**………………………………………..**

**LEVINA B. LUBANZIBWA  MKUU WA SHULE**

Tafadhali jaza sehemu hii hapa chini kukiri kwamba umesoma na kuelewa maelekezo ya fomu hii. Hivyo kusaini kwako hapa inachukuliwa kwamba umekubaliana na sheria/taratibu zote za mwanao kuwepo hapa shuleni.

**KUKIRI,**

Jina la mtoto……………………………………………………

Jina la mzazi……………………………………………………

Sahihi ya mzazi…………………………………………….

Na. simu (mzazi/mlezi)…………………………………….

## KIAMBATANISHO KWA WANAFUNZI WA HOSTEL

Uongozi wa shule unayofuraha kukutaarifu kwamba mwanao amepangiwa kukaa hostel. Mzazi utawajibika kutimiza wajibu wako kuzingatia maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari Mbondole, hii ni pamoja na matibabu ya mwanao, nauli ya kwenda nyumabani na kurudi shule wakati wa likizo na vifaa vya kutumia awapo shuleni.

Uhitaji wa Hostel ni makubwa hivyo mwanao hataendelea kuishi Hostel ifikapo mwisho wa mwaka endapo atashindwa kutimiza masharti, vigezo na taratibu za Hostel kama ifuatavyo ;

1. Mtoto atawajibika kupata ufaulu wa daraja la **KWANZA** hadi la **TATU** ifikapo mwisho wa mwaka wa masomo. Wastani huu ni majumuisho ya mitihani na majaribio yote ya mwaka husika
2. Mawasiliano yote kati ya mzazi/mlezi na mwanafunzi yatafanyika kupitia kwa mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule au mwalimu mlezi wa hostel
3. Mzazi atawajibika kuacha mawasiliano ya simu ambayo itapatikana muda wote na hataruhusiwa kufika shuleni kuonana na mwanafunzi isipokuwa siku maalumu ya kumtembelea mwanafunzi ambayo itapangwa na uongozi wa shule na taarifa zitawafikia wazazi/walezi
4. Mtoto atawajibika kufuata masharti na taratibu zote atakazopewa awapo Hostel
5. Kila mzazi ahakikishe kuwa mtoto amekatiwa **BIMA YA AFYA** kwa ajili ya matibabu

## VIFAA VYA HOSTEL

1. Sahani, bakuli, kikombe vyote vya plastiki rangi ya bluu
2. Jozi za kandambili, taulo la kuogea, shuka mbili rangi ya PINK, mto (pillow) yenye foronya ya pink, chandarua nyeupe, tandiko (godoro) la **futi 3**
3. Tracksuit rangi ya bluu, raba za michezo na shamba dress rangi ya kahawia (**rangi utakayopewa shuleni)**
4. Mafuta ya kujipaka yasiyo na manukato (**perfumes haziruhusiwi**), mswaki, dawa ya meno na taulo za kike (sanitary pads)
5. Ndoo ya lita 10, ufagio (soft broom) mopa na ndoo yake, ufagio wa chooni (hard broom)
6. Trucker la chuma na kufuli.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMUONDOA MWANAFUNZI HOSTEL

1. Kuvunja sheria za shule
2. Uchafu wa mwili, nguo na vyombo anavyotumia
3. Kuvaa nguo zisizo ruhusiwa kwa wakati unaotakiwa au kuvaa mavazi ambayo hayafuati maadili. (**nguo fupi na zinazobana au kaptura**)
4. Kushindwa kuhudhuria masomo/maandalizi ya masomo usiku kwa muda unaotakiwa na kusumbua wenzie kwa kupiga makelele au kulala badala ya kusoma

5. Kushindwa kuungana na wenzie katika sala au maombi kabla ya masomo/maandalizi ya masomo ya usiku wakati wa kuanza na wakati wa kwenda kulala
6. Kuanzisha vikundi/magenge yasiyo na mwelekeo wa kimasomo
7. Kuiba mali za wenzie bwenini
8. Kusingizia kuumwa kusudi apate fursa ya kutofanya mitihani au kurudi nyumbani
9. Kushindwa kupata wastani wa alama za masomo unaokubalika kwa wanafunzi wa Hostel
10. Mzazi kutokuhudhuria vikao viwili mfululizo vya wazazi wenye watoto Hostel na vya shule kwa ujumla.

Mwisho mzazi unatakiwa kukiri kwamba unakubali masharti na taratibu hizi zote na upo tayari kukubali mwanao kuondolewa hostel endapo masharti yamekiukwa na wewe mwenyewe au mtoto kama ilivyo elekezwa

Pia unatakiwa kuhudhuria vikao vyote vya shule na vya wazazi wenye watoto Hostel. Hivyo kusaini kwako hapa inachukuliwa kwamba umekubaliana na sheria/taratibu zote za mwanao kukaa Hostel.

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

| **PICHA YA<br>MZAZI/MLEZI** |
|---|

Mimi mzazi/mlezi wa (jina la mtoto)……………………………………………..nakiri kwamba

nimesoma na kuelewa kanuni/taratibu na sheria za shule kwa ajili ya mwanangu awapo Hostel / shuleni, hivyo nitakuwa tayari kukubaliana na maamuzi yoyote yatakayo chukuliwa na uongozi wa shule endapo mwanangu atakiuka kanuni/taratibu na sheria zilizo ainishwa hapo juu.

Jina la mzazi ………………………………………………………………

Sahihi ya mzazi ……………………………………….

Na. simu mzazi/mlezi) …………………………………………………

**KIAMBATANISHO A PRESIDENTS OFFICE-**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL**
GOVERNMRNT **AUTHORITIES**

To be completed by a governmental medical officer

……………………………………………………

……………………………………………………

…………………………………………………… date ………………..

RE: …………………………………………………………………………………………

Please examine the person mentioned above and comment on his or her health responsible to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either **YES** or **NO**.

Does a students has a problem in connection with

a) Sight ………………………………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

b) Hearing ……………………………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

c) Speech ……………………………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

d) Blood pressure……………………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

e) T.B ………………………………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

f) Any physical disability …………… 1. NO ☐ YES

   If yes, state …………………………………………………………………………

   If yes, state …………………………………………………………………………

g) Do you therefore, recommend the said students medically fit; in for studentship at this institution? …………………………... 1. NO ☐ YES

Reasons. ………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………...

Date ……………..…….. Name …………………………….. Signature ………………..

Designation stamp …………………………………